



**MWITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI NA
LESENI KUTOKA EWURA.**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoungwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 126 (1) cha sheria hiyo kinamtaka mtu yoyote anayetaka kujenga miundombinu ya mafuta kuomba kibali cha ujenzi kutoka EWURA. Aidha, Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

EWURA imepokea maombi ya vibali vya ujenzi na leseni kutoka kwa waombaji walioorodheshwa hapa chini. Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba vibali vya ujenzi ili wajenge miundombinu ya mafuta na leseni kwa ajili ya kujihusisha na biashara/shughuli katika mkondo wa kati na chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

S/N	Jina la Mwombaji	Eneo	Jina la Mkurugenzi/Uraia	Aina ya Ombi la Leseni/Kibali cha Ujenzi
1	ELIAS TRANSPORT COMPANY LIMITED, 63104-02-012-0037, MTWARA	Kiwanja Na. 407, Kitalu Na. J, SHANGANI, MTWARA, MTWARA	ELIA BACHU RAMIN	Kibali cha ujenzi wa Kituo cha Mafuta
2	MUSSA SINAHOFU BOMEZA, 12114-09-232-0261, Dar es Salaam	Kiwanja Na. 12, Kitalu Na. D, MSONGOLA, ILALA, Dar es Salaam	MUSSA SINAHOFU BOMEZA	Kibali cha ujenzi wa Kituo cha Mafuta

Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote aliyetajwa hapo juu kwamba asipewe leseni au Kibali cha ujenzi, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.

**Imetolewa na
Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**